3	Kukosekana kwa wadau wengine katika warsha	Wadau wafuatao washirikishwe katika warsha; Sekta za Kilimo, Maji, Madini, Mifugo na Wanyamapori na Wakuu wa Mikoa ya Ruvuma, Pwani na Mtwara	MCDI, WWF na MJUMITA	TAMISEMI, TAWA, AAC na TFS	Katika Warsha hii Wadau wa Sekta ya Madini, na Wanyamapori wamealikwa. Pia Wakuu wa Mikoa ya Pwani na Ruvuma walialikwa ila kutokana na majukumu mengine muhimu hawajaweza kufika. Wadau wengie wataendelea kualikwa katika Warsha zijazo.
4	Uhaba wa masoko ya mazao ya misitu	Halmashauri na TFS kwa kushirikiana na wadau waandae na kutekeleza mipango maalumu ya kutafuta masoko ya mazao ya misitu katika maeneo yao	Wakurugenzi wa Halmashauri na TFS	MCDI, WWF, MJUMITA na TFS	Tatizo la Masoko limeendelea kutatuliwa kwa kutafuta wateja zaidi wa Rasilimali za misitu
5	Kutokuwa na udhibiti wa mifugo inayoingia mikoa	Kuwe na mpango wa pamoja wakutathimini na kudhibiti uingizaji wa mifugo	Ofisi ya Mkuu wa Mikoa wa Lindi/ Wakuu	MCDI, WWF, TFS, MJUMITA na sekta ya	Utatuzi wa Migogoro ya Wafugaji na Wakulima imekuwa ikifanyika. Mikutano ya Wadau wa Mifugo imekuwa ikifanyika kila mwaka ili

<b>NA</b>	<b>HOJA</b>	<b>MAAZIMIO</b>	<b>MHUSIKA</b>	<b>WADAU</b>	<b>UTEKELEZAJI</b>
	ya Pwani, Lindi, Mtwara na Ruvuma	katika mikoa ya Pwani, Lindi, Ruvuma na Mtwara pamoja na Wilaya zake	wa Wilaya	mifugo, ardhi na kilimo	kutatua changamoto za muingiliano wa matumizi ya ardhi. Hata hivyo changamoto hii bado ipo na Serikali inaendelea kulitua jambo hili.
6	Kukosekana kwa motisha kwa wanakamati wa vijiji ambavyo havipati mapato kutokana na rasilimali misitu	Kuwezesha vijiji kuandaa mipango ya kuongeza vyanzo vya mapato ili kuboresha motisha kwa kamati za maliasili	Halmashauri za Wilaya, WWF, MCDI, MJUMITA na TFS	Taasisi mbalimbali za utafiti na Wadau wengine wa maendeleo	Kamati za maliasili na vikundi vya Jamii vinawezeshwa ili kupanua vyanzo vya mapato. Kwa mfano, Wilaya ya Liwale vikundi na mtu mmoja mmoja kupitia mradi wa FORVAC vinawezeshwa kwa kuanzisha miradi biashara ndogondogo.,
7	Kutokuwepo kwa mahusiano mazuri katika utekelezaji wa majukumu mionganini mwa watendaji katika sekta ya misitu	Mahusiano mionganini mwa watendaji katika sekta ya misitu yaboreshwe kwakuweka utaratibu mzuri wa mawasiliano na ushirkiano mionganini mwa watendaji kwakuzingatia randama ya makubaliano baina ya TAMISEMI na MNRT	Halmashauri za Wilaya na TFS	Mashirika yasiyo yakiserikali	Mahusiano yameendelea kuimarishe kuitia vikao mbalimbali vya utekelezaji na kuitia Randama
8	Maeneoa valiyovunwa /kuathiriaka kutopewa kiapaumbele katika upandaji miti	Asilimia 5% ya tozo ya upandaji miti inayorejeshwa Halmashauri kutoka TAFF kwa ajili ya kuendeleza upandaji miti ielekezwe katika vijiji ambavyo uvunaji umefanyika na maeneo ambayo yamethirika na uharibifu wa mazingira.	Halmashauri za Wilaya na TFS	Mashirika yasiyo yakiserikali na watu binafsi	Jitihada ya kuomba 5% ya tozo bado zinaendelea ingawa upandaji miti unaendelea kuitia mapato ya ndani ya Halmashauri

<b>NA</b>	<b>HOJA</b>	<b>MAAZIMIO</b>	<b>MHUSIKA</b>	<b>WADAU</b>	<b>UTEKELEZAJI</b>
9	Kutokuwepo kwa utawala bora na usimamizi wa rasilimali fedha	Yatolewe mafunzo na tathimini ya utawala bora katika ngazi zote za Halmashauri za Wilaya juu ya uadilifu, uzalendo na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za misitu	Halmashauri na MJUMITA	MCDI,TFS,na WWF	Mafunzo ya Utawala Bora katika Usimamizi wa rasilimali fedha yametolewa na Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na Shirika la MJUMITA. Kwa mfano Kilwa, Liwale, Ruangwa, Tunduru, Namtumbo na Rufiji)
11	Vijiji kutonufaika na uwepo wa wanyama pori	Vijiji vyenye maeneo yenyewe wanyamaporini visaidiwe kuanzisha WMA, ili viweze kunufaika na rasilimasli ya wanyama pori kama ilivyo kwa vijiji vinavyo nufaika na utekelezaji wa dhana ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu	Halmashauari	WWF, TFS, MCDI na MJUMITA	Jitihada zinaendelea kufanyika kwa baadhi ya Wilaya kwa kuandaa maandiko ya lutafuta wadau mbalimbali wa kuwezesha WMA
12	Uharibifu unaosababishwa na kilimo cha kuhamahama	Kutoa elimu endelevu juu kilimo hifadhi kinacholenga kupunguza uharibifu wa misitu kwa wakulima vijijini	Halmashauari		Elimu juu ya Kilimo Hifadhi Hifadhi imeendelea kutolewa na Halmashauri zinaendelea kuandaa matumizi bora ya ardhi ya vijioji.
13	Kutokwepo kwa motisha katika vijiji vinavyo fanya vizuri	Vijiji vinavofanya vizuri katika suala la utawala bora vipatiwe tuzo kuongeza motisha kwa vijiji vingine.	Halmashauari	MJUMITA, WWF, MCDI, Action Aid na TCRS	Motisha umeanza kutolewa kwa vijiji vinavyofanya vizuri. Mfano Kijiji cha Sautimoja kilichopo Tunduru. Zoezi hili ni endelevu
14	Uelewa mdogo kuhusu uthibitishaji wa misitu.	Wadau wote, wanaohusika na usimamizi wa misitu wajengewe uwezo kuhusu uthibitishaji wa mazao ya	MCDI	Halmashauri za wilaya, TFS na wafanya biashara wa	Mafunzo ya ya Uthibitishaji misitu yametolewa kwa vijiji vyote vinavyofanya kazi na MCDI, zoezi hili ni endelevu.

<b>NA</b>	<b>HOJA</b>	<b>MAAZIMIO</b>	<b>MHUSIKA</b>	<b>WADAU</b>	<b>UTEKELEZAJI</b>
		misitu.		mazao ya misitu	Pia ya kuwajengea uwezo watumishi wa Serikali (TFS na Halmashauri za Wilaya katika Mikoa ya Lindi. Ruvuma na Pwani) ilifanyika mwaka mwaka 2018 kuwajengea uwezo juu ya Uthibitishaji misitu.
15	Kutokuwa na warsha endelevu	Kuwe na warsha ambazo ni endelevu kuhusu masuala ya Uhifadhi wa Misitu.	Halmashauri za Wilaya, MCDI, WWF na TFS	Washiriki wa warsha	Warsha zinaendlea kufanyika na kuongeza wigo wa Washiriki

## **Appendix. 4. Village presentations (Swahili)**

### **TAARIFA YA MAENDELEO YA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU WILAYA YA NAMTUMBO**

#### **A. UTANGULIZI**

Mh. Mgeni rasmi

Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ni mionganini mwa wilaya tano zilizopo mkoa wa Ruvuma. Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na mashirika ya WWF, MJUMITA na MCDI ilianza Mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu kwa Jamii Julai 2016 na kutenga maeneo ya msitu yenye jumla ya hekta za eneo la msitu 20,789 katika ardhi ya vijiji 2 vya Mtawamwahi hekta 8,859 na Kitanda hekta 11,930. Baadae mwaka 2020 Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kwa kushirikiana na MCDI kuitia program ya FORVAC imewezesha vijiji 4 kuanzisha hifadhi ya misitu ambapo kijiji cha Limamu kimetenga eneo la msitu lenye hekta 16,391. Kazi ya kutenga misitu ya Vijiji vya Kilangalanga, Chengena na Masuguru inaendelea.

#### **B. MAFANIKIO**

Mh. Mgeni rasmi, yafuatayo ni mafanikio yaliyopatikana katika usimamizi shirikishi wa misitu katika wilaya ya Namtumbo.

Kijiji cha Mtawamwahi kilipata jumla ya shilingi 2,990,000/= kutokana na mauzo ya magogo. Pesa hizo zilitumika kumalizia ujenzi wa vyoo vya shule ya msingi ya Mtawamwahi.

Kijiji cha Kitanda hakikuweza kupata mteja yeyote bali kilivuna miti na kupata mbao 89 zenye thamani ya Tsh 1,673,900/- ambazo zilitumika kutengenezea milango na madirisha ya Zahanati ya kijiji.

Pamoja na mafanikio hayo pia vijiji vimepata elimu juu ya; -

- Utawala bora
- Utunzaji wa nyaraka mbalimbali
- Uhifadhi endelevu wa misitu unaotokana na usimamizi shiriki.

<b>S/N</b>	<b>CHANGAMOTO</b>	<b>JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA</b>	<b>MAPENDEKEZO</b>
<b>1</b>	Kukosekana kwa soko la mazao ya misitu	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Vijiji kuendelea kukaa na wafanya biashara katika kuelezea ubora na wingi wa rasilimali zao zilizopo katika misitu ya hifadhi ya vijiji.</li> <li>• Kushirikisha wadau mbalimbali katika kutangaza soko la mazao ya misitu iliyopo katika misitu ya vijiji.</li> </ul>	<p>a. Halmashauri ya wilaya pamoja na Programu ya FORVAC, mashirika ya WWF, MCDI na wadau wengine wasaidie kutafuta masoko ya mazao ya misitu yanayopatikana kwenye misitu ya Vijiji..</p> <p>b. Kamati za Maliasili kujengewa uwezo na mbinu za kutafuta Masoko ya mazao ya misitu.</p>
2	Kukosekana kwa vyombo vya usafiri kwa kamati za maliasili za vijiji.	Katika bajeti na mipango kazi ya mwaka, vijiji vimeweka bajeti kwa ajili ya kununua vyombo vya usafiri vitakavyotumika katika shughuli za usimamizi shirikishi wa misitu.	Serikali na wadau wasaidie kutafuta wateja wa mazao ya misitu ili kupata fedha ya ununzi wa vyombo vya usafiri.

## **TAARIFA YA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU YA JAMII WILAYA YA TUNDURU**

### **A: UTANGULIZI**

Mh. Mgeni rasmi

Halmashauri ya wilaya ya Tunduru ni mionganini mwa wilaya tano zilizopo mkoa wa Ruvuma. Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na mashirika ya WWF, MCDI, MJUMITA mwaka 2014 na baadae mwaka 2020 Programu ya FORVAC waliweza kuanzisha Mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu ya Jamii. Jumla ya hekta za misitu 77,906 zimetengwa kwenye viji 9 ambavyo ni Mindu, Ngapa, Sautimoja, Machemba, Songambele, Msinji, Liwangula, Kajima na Namakambale. Hata hivyo kazi ya kutenga msitu mpya inategemewa kuendelea katika kijiji cha Mbungulaji

### **B. MAFANIKIO**

Mh. Mgeni rasmi, yafuatayo ni mafanikio yatokanayo na usimamizi shirikishi wa misitu;

1. Mpaka hivi sasa viji vya wilaya ya Tunduru vimeweza kuvuna kiendelevu jumla ya mita za ujazo 726 kwa kuuza magogo na kuweza kukusanya jumla ya Mapato Tshs 168,408,000/=. Kati ya mapato yaliyopatikana Asilimia 40 ya mapato yametumika kuimarisha shughuli za usimamizi wa msitu, 10% ni gawio kwa Halimashauri ya wilaya ya Tunduru katika kuimarisha huduma za Kitaalamu na 50% zimetumika kutekeleza shughuli za maendeleo za viji husika.
2. Katika kuongeza thamani ya mazao ya misitu, viji vilianza kufanya biashara ya mbao badala ya kuuza magogo. Mfano kijiji cha Sautimoja kimeweza kuvuna magogo yenye mita za ujazo 125 na kuyachakata kwa Mashine ya kisasa inayohamishika na yenye ufanisi mkubwa iliyopatikana kuititia ufadhili wa WWF na kuwezesha kupata Mapato ya Tshs 87,370,000/= yaliyotokana na kuuza mbao. Kama Kijiji kingeza magogo pekee kingejipatia Tshs 32,500,000/= tu. Hivyo kijiji kimeweza kupata faida ya (Tshs 19,333,700/= 59.5%) kwa mauzo ya mbao na Tsh 7,609,000/= (23.4%) kwa mauzo ya mabaki). Kutokana na Mashine kuwa na ufanisi wa kupunguza upotevu wa gogo kwa 57% umesaidia kupunguza idadi ya miti iliyovunwa ambapo kama ingetumika teknolojia ya zamani wangevuna mara mbili ya idadi ya miti ili yunwa.
3. Kupatikana kwa nafasi 165 za ajira za muda mfupi kwa wanajamii kipindi cha uchakataji wa magogo na usafirishaji. Aidha wanajamii 2 kutoka kijiji cha Sauti moja wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya namna ya kutumia mashine hiyo.
4. Kuimarika kwa utawala bora kutokana na ukaguzi wa fedha za viji kutoka kwa mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya wilaya wakishirikiana na MJUMITA.

5. Vijiji vimeweza kutengeneza samani za ofisi ambazo zimepelekeea utunzaji mzuri wa kumbukumbu na nyaraka mbalimbali (Mindu na Namakambale).
6. Kijiji cha Sautimoja kimechangia Matofali 3000 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mtendaji wa kijiji na kujenga darasa moja jipya la shule ya msingi Sautimoja.
7. Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa ya shule ya Msingi Namakambale
8. Vijiji vimeweza kujenga ofisi za vijiji (Ngapa,Sautimoja, Machemba na ukarabati Namakambale).
9. Vijiji vimenunua pikipiki kwa ajili ya shughuli za usimamizi shirikishi wa msitu (Machemba, Ngapa na Sautimoja).
10. Kijiji cha Machemba wamejenga soko la kisasa na ghala.

**C. CHANGAMOTO, JITIHADA PAMOJA NA MAPENDEKEZO**

**Mh. Mgeni rasmi zifuatazo ni changamoto, jitihada pamoja na mapendekezo**

<b>S/N</b>	<b>CHANGAMOTO</b>	<b>JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA</b>	<b>MAPENDEKEZO</b>
<b>1</b>	Uhaba wa wateja wa mazao ya misitu.	Vijiji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya na wadau wengine wanaendelea kutafuta Masoko kwa kutumia njia mbalimbali kwa mfano mitandao ya kijamii na mikutano mbalimbali.	Wadau mbalimbali wawezeshe mtaji wa kuanzia kuchakata mazao ya misitu ili kuongeza thamani.  Uanzishwaji wa karakana za useremala kwa vijana ambao watatumia rasilimali misitu
<b>2</b>	Ukosefu wa mtambo wa kukaushia mbao unaotumia nishati ya jua (Solar Kiln).	Vijiji vimepeleka maombi ya uhitaji wa mtambo wa kukaushia mbao unaotumia nishati ya jua kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.	Serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo wasaidie upatikanaji wa mtambo.
<b>3</b>	Kukosekana kwa mafunzo ya ujasiri na nyenzo kwa Kamati za Maliasili kwa ajili ya kukabiliana na wafugaji, wavunaji haramu wa magogo na majangili wanaovamia misitu ya hifadhi ya Vijiji.	Kamati za maliasili zinashirikisha askari wanyama pori wanapotekeleza shughuli za usimamizi wa msitu japokuwa ni gharama kubwa kwa kijiji.	Kamati za maliasili zipatiwe mafunzo ya jeshi la akiba (mgambo) ili ziweze kukabiliana na wimbi la wafugaji, wavunaji haramu pamoja na majangili.
<b>4</b>	Kukosekana kwa vyombo vyaa usafiri kwa kamati za maliasili za vijiji wakati wa shughuli za usimamizi wa misitu.	Kamati za maliasili zinakodi, kutumia vyombo binafsi au kutembea kwa miguu pale inapohitajika.	Serikali na wadau mbalimbali wasaidie kutafuta wateja wa mazao ya misitu ili kupata fedha za kununua vitendea kazi.

## **TAARIFA YA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU YA JAMII HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA**

### **A: UTANGULIZI**

Mh. Mgeni rasmi

Wilaya ya Songea ni mionganini mwa Wilaya tano zilizopo mkoa wa Ruvuma. Halmashauri ya Wilaya, kwa kushirikiana na Halmashauri za Vijiji vya Litowa, Liweta, Ndongosi, Kitulo na Muhukuru-Lilahi katika program ya KILIMO MSETO zilifanikiwa kutenga misitu yenyeye jumla ya hekta 17,085 mwaka 2012. Baadae mwaka 2020 Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na MCDI kuititia Programu ya kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao ya misitu (FORVAC) ziliendeleza shughuli za usimamizi shirikishi wa misitu.

### **B: MAFANIKIO**

Mh. Mgeni rasmi,

Yafuatayo ni Mafanikio yaliyopatikana katika vijiji vitano (5) vinavyo tekeleza dhana ya usimamizi shirikishi wa Misitu;

11. Kuongezeka kwa uelewa wa wanajamii kuhusu uhifadhi wa misitu kuititia mafunzo yaliyotolewa na Halmashauri ya wilaya ya Songea kwa kushirikiana na Chuo cha Kilimo cha Sokoine na MCDI.
12. Halmashauri ya Wilaya ya Songea kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kuititia Programu ya FORVAC wamewezesha vijiji kufanya Tathimini shirikishi ya rasilimali za misitu katika misitu ya hifadhi ya vijiji na kuandaa mipango ya Usimamizi shirikishi na uvunaji endelevu ya mazao ya misitu

**C: CHANGAMOTO, JITIHADA NA MAPENDEKEZO ILI KUTATUA CHANGAMOTO HIZO**

S/N	CHANGAMOTO	JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA	MAPENDEKEZO
1	Vijiji kutokuwa na uelewa wa kutosha wa namna ya kuunganishwa na wateja wa mazao ya misitu	Fursa ya kuuza mbao kwenye miradi ya ujenzi wa shule zimepatikana kwa uchache.	Serikali pamoja na wadau mbalimbali wasaidie kuunganisha Vijiji na wateja wa mazao ya misitu
2	Uvamizi wa wakulima kwenye misitu ya hifadhi ya vijiji vya Muhukuru- Lilahi, Liweta na Litowa.	Kamati za maliasili zimefanya doria za mara kwa mara ili kukabiliana na uvamizi wa wakulima ndani ya Misitu ya hifadhi ya vijiji.	Serikali kupitia kamati ya usalama ya wilaya isaidie kuwatoa wakulima waliovamia hifadhi ya misitu
3	Uhaba wa vitendea kazi wakati wa shughuli za usimamizi wa misitu kama vile GPS, pipipi, sare za wanakamati ya maliasili, na sanduku la huduma ya kwanza kwa kuwa vijiji bado havijavuna na kuuza mazao ya misitu.	Kamati za maliasili zimekuwa zikijitolea bila kuwa na vitendea kazi na kutumia njia za asili na watu wenye uzoefu wa maeneo ya misitu katika kufanya shughuli za usimamizi wa misitu.	Serikali na wadau mbalimbali wasaidie kutafuta wateja wa mazao ya misitu ili kupata fedha ya ununuzi wa vitendea kazi.
4	Mgogoro wa mpaka kati ya kijiji cha Ndongosi na Muhukuru-Lilahi ambao umepelekea ucheleweshwaji wa zoezi la utengaji wa msitu wa hifadhi katika kijiji cha Muhukuru- Lilahi.	Vijiji viwili vimekutana kwa ajili ya kusuluuhisha mgogoro huu pasipokuwa na mafanikio.	Serikali ya Wilaya iingilie kati ili kusaidia kutatua mgogoro huu.

## **MAWASILISHO YA VIJIJI VYA WILAYA YA RUFIFI KATIKA WARSHA YA WADAU WA MISITU**

### **A. UTANGULIZI**

Mh. Mgeni rasmi

Ifuatayo ni taarifa fupi ya maendeleo ya vijiji vinavyotekeleza usimamizi shirkishi wa misitu ya jamii katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji mkoa wa Pwani. Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na shirika la kuhifadhi Mpingo na maendeleo (MCDI) kuitia ufadhili wa WWF ilianza utengaji wa misitu na uandaaji wa Mipango ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu 2 kati ya mwaka 2006 hadi 2020. Jumla ya hekta 4,431 zimehifadhiwa kwenye vijiji 2 ambavyo ni Tawi na Nyamwage.

### **B. MAFANIKIO**

Mh. Mgeni rasmi, yafuatayo ni mafanikio yaliyopatikana mpaka hivi sasa:

1. Kutokana na biashara ya magogo kutoka kwenye misitu ya hifadhi ya vijiji, jumla ya mita za ujazo 89.72 zimevunwa na kupata jumla ya shilingi 19,198,000/=.  
Kati ya mapato yaliyopatikana, 40% ya mapato imetumika kutekeleza shughuli za usimamizi wa misitu, 5% ni gawio kwa Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya huduma za kitaalamu na 55% imetumika kutekeleza shughuli za maendeleo vijijini.
2. Kijiji cha Nyamwage kilitengeneza meza 14 na viti 14 kwa ajili ya ofisi ya walimu kwa shule za msingi Nyamwage na Shauri moyo
3. Kugharamia kukarabati miundombinu ya kisima cha maji katika Kijiji cha Nyamwage.
4. Kuimarika kwa usimamizi wa fedha katika Kijiji cha Tawi kutokana na ukaguzi wa fedha za kijiji kutoka kwa mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya wilaya wakishirikiana na MJUMITA.
5. Kuchangia ujenzi wa darasa moja la shule ya msingi Tawi.

**C. CHANGAMOTO, JITIHADA ZILIZOFANYIKA NA MAPENDEKEZO**

**Mh. Mgeni rasmi, pamoja na mafanikio hayo, bado Vijiji hivi vinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:**

S/N	CHANGAMOTO	JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA	MAPENDEKEZO
1	Uhaba wa masoko ya uhakika ya mazao ya misitu	Vijiji vimejisajili kama wafanyabiashara wa mazao ya misitu ili kuweza kuvuna na kuchakata mbao.	<ul style="list-style-type: none"> <li>a. Wadau mbalimbali wajitokeze kufadhili vijiji ili viweze kugharamia uchakataji wa mbao kutoka katika misitu ya vijiji.</li> <li>b. Serikali na wadau wajengee uwezo kamati za Maliasili ili kuwa na uwezo wa kuitangaza zaidi miti isiyofahamika.</li> </ul>
2	Upungufu wa vitendea kazi kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa msitu.	Wanakamati hujitolea vitendea kazi wakati wa kutekeleza shughuli za usimamizi shirikishi wa misitu.	Serikali na wadau mbalimbali wasaidie kutafuta wateja wa mazao ya misitu ili zipatikane fedha za ununzi wa vitendea kazi.
3	Uvunaji haramu na Uvamizi wa wafugaji ndani ya hifadhi ya misitu.	Vijiji vinaendelea kufanya doria mbalimbali kukabiliana na wafugaji na wavunaji haramu.	<ul style="list-style-type: none"> <li>a. Wanakamati wapatiwe mafunzo ya jeshi la akiba (mgambo) ili waweze kufanya doria kwa ufanisi zaidi.</li> <li>b. Kufanyika kwa Doria shirikishi kisekta ili kutatua tatizo hili.</li> </ul>

## **TAARIFA YA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU YA JAMII WILAYA YA NACHINGWEA**

### **A: UTANGULIZI**

Mh. Mgeni rasmi

Ifuatayo ni taarifa fupi ya maendeleo ya vijiji juu ya utekelezaji wa usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii katika Halmashauri ya wilaya ya Nachingwea, mkoa wa Lindi.

Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii ulianza kutekelezwa mwaka 2004, Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na mashirika ya FINIDA, WWF, TFCG, MCDI na baadaye Programu ya FORVAC (2019). Jumla ya Hekta za misitu **40,901** zimehifadhiwa kisheria kwenye ardhi za vijiji nane (8) ambavyo ni *Mbondo, Kilimarondo, Majonanga, Nanjih, Namatunu, Kiegei B, Lionja B na Ngunichile*. Vijiji hivi nane vipo katika programu ya kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu (FORVAC).

### **B: MAFANIKIO**

Mh. Mgeni rasmi, yafuatayo ni mafanikio yatokanayo na usimamizi shirikishi wa misitu;

1. Vijiji vimechangia katika sekta ya Afya:

- i. Kijiji cha Ngunichile kimechangia kiasi cha takribani Tsh 48,000,000/= kwenye ujenzi wa kituo cha afya cha Ngunichile.
- ii. Kijiji cha Lionja "B" kimechangia kiasi cha takribani Tsh 2,500,000/= kwenye ujenzi wa zahanati ya kijiji.
- iii. Kuweka umeme wa sola kwenye zahanati ya kijiji cha Ngunichile wenye thamani ya Tshs 2,200,000/=
- iv. Kijiji cha Lionja B wamechangia kiasi cha 1,500,000/= kuweka umeme wa TANESCO kwenye zahanati ya kijiji.

2. Vijiji vimechangia katika sekta ya Elimu:

- i. Ujenzi wa madarasa 3 kwa shule ya msingi Namatunu na darasa 1 shule ya Sekondari Lionja.
- ii. Ujenzi wa maabara ya shule ya sekondari ya Mbondo, vyoo 3 vyenye jumla ya matundu 22 katika shule za msingi za Lionja B, Majonanga na Mbondo.
- iii. Kuweka umeme wa sola kwenye madarasa 2 ya shule ya msingi na nyumba za walimu 7 katika kijiji cha Ngunichile.
- iv. Kutengeneza madawati 97 na kukarabati madawati 30 katika shule ya msingi Kiegei B.

3. Ujenzi wa ofisi za vijiji vya Majonanga na Namatunu.

4. Vijiji vinachangia asilimia 15 ya mapato ya msitu kwa ajili ya huduma za kitaalamu zitolewazo na Halmashauri ya Wilaya.
5. Ujenzi wa mabanda manne (4) ya biashara kwa ajili ya kupangisha ili kuongeza pato la kijiji (Kijiji cha Ngunichile ) na kutengeneza meza 8 na benchi 8 kwa ajili ya kuongeza pato kupitia ushuru wa soko la kijiji cha Mbondo.
6. Ununuzi wa vitendea kazi kwa kamati za maliasili kwa ajili ya shughuli za usimamizi shirikishi wa misitu (Sare jozi 12 Ngunichile, hema 1 Mbondo, pikipiki 2 (Mbondo na Ngunichile, baiskeli (4 Majonanga, 3 mbondo na 1 Ngunichile) .
- 7.Kijiji cha Lionja B kimeweza kujigharamia jumla ya shilingi 3,000,000/= katika kufanya tathimini shirikishi ya rasilimali msitu katika msitu wa hifadhi wa kijiji na kuandaa mpango shirikishi wa usimamizi na uvunaji endelevu.
8. Kijiji cha Mbondo kimechangia katika ujenzi wa masjala ya ardhi jumla ya Tshs 3,782,000/=

**C: CHANGAMOTO , JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA NA MAPENDEKEZO**

**Mh. Mgeni Rasmi** zifuatazo ni changamoto, Jitihada zilizochukuliwa na mapendekezo katika kutatua changamoto hizo:

S/N	CHANGAMOTO	JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA	MAPENDEKEZO
1	Uhaba wa masoko ya uhakika ya mazao ya misitu hasa kwa jamii ya miti isiyofahamika	<ul style="list-style-type: none"> <li>Vijiji kuendelea kukaa na wafanya biashara katika kuelezea ubora na wingi wa rasilimali zao zilizopo katika misitu ya hifadhi ya vijiji.</li> <li>Kushirikisha wadau mbalimbali katika kutangaza soko la mazao ya misitu iliyopo katika misitu ya vijiji.</li> </ul>	Serikali itoe kipaumbele kununua mazao ya misitu kutoka kwenye misitu ya hifadhi ya vijiji katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili kukuza soko la ndani la mazao ya Misitu.
2	Uvamizi wa Mifugo, wakulima na wavunaji haramu ndani ya misitu ya hifadhi ya vijiji	Vijiji vimefanya doria mbalimbali kukabiliana na wafugaji, wakulima na wavunaji haramu ndani ya Misitu ya hifadhi ya vijiji.	<p>(a)Kamati za maliasili zipatiwe mafunzo ya mgambo, hii itasaidia kujilinda na uvamizi wa wafugaji, wakulima na wavunaji haramu ndani ya misitu ya hifadhi ya vijiji.</p> <p>(b)Serikali kuweka kituo cha ukaguzi cha maliasili kwenye barabara itokayo Kilimarondo kupitia mbondo kwenda Nachingwea mjini.</p>
3	Uhaba wa vitendea kazi katika shughuli za usimamizi wa misitu kama vile mahema, GPS na Sare za kamati za maliasili wakati wa shughuli za usimamizi shirikishi wa misitu.	Vijiji vimeandaa bajeti za vitendea kazi katika mipango kazi ya mwaka.	Serikali na wadau mbalimbali watusaidie kutafuta wateja wa mazao ya misitu ili tuweze kupata fedha ya ununuzi wa vitendea kazi hivyo.
4	Kuongezeka kwa matukio ya moto	Vijiji vinaendelea kuweka barabara za	Kamati za maliasili za vijiji zipatiwe

<b>S/N</b>	<b>CHANGAMOTO</b>	<b>JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA</b>	<b>MAPENDEKEZO</b>
	kichaa ndani na nje ya misitu ya hifadhi ya vijiji.	kuzuia moto pembezoni mwa misitu ya hifadhi ya vijiji.	mafunzo ya ubabuaji ili kupunguza matukio ya moto kichaa kipindi cha kiangazi.

## **TAARIFA YAUSIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITUYA JAMII WILAYA YA KILWA**

### **A. UTANGULIZI**

Mh. Mgeni rasmi

Ifuatayo ni taarifa fupi ya maendeleo ya vijiji vinavyotekeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya jamii katika Halmashauri ya wilaya ya Kilwa mkoa wa Lindi. Kwa kushirikiana na mashirika ya WWF, MCDI na MJUMITA. Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii ulianza kutekelezwa mwaka 2004. Jumla ya Hekta 163,260.72 zilishatengwa kwenye vijiji 13 (Nanjirinji A, Nanjirinji B, Mchakama, Namatewa, Ngea, Kikole, Kisangi, Kipindimbi, Nainokwe, Liwiti, |Somaga Simu , Marendego na Likawage).

### **B. MAFANIKIO**

Mh. Mgeni rasmi

1. Kutokana na biashara ya uuzaaji magogo kutoka kwenye misitu ya hifadhi ya vijiji 13 vya wilaya ya Kilwa, jumla ya mita za ujazo 8904.88 zimevunwa na kuuzwa na kuweza kupata jumla ya Mapato ya shilingi Bilioni 1.8 toka mwaka 2009 hadi 2020. Kati ya mapato yaliyopatikana Asilimia 40 ya mapato imetumika katika kuimarisha usimamizi shirikishi wa shughuli za msitu, 5% imetumika katika kuimarisha huduma katika halmashauri ya wilaya ya Kilwa na 55% imetumika katika shughuli za maendeleo vijijini.
2. Katika kuongeza thamani ya mazao ya misitu vijiji vimeanza biashara ya kuuza mbao badala ya kuuza magogo. Vijiji vya Ngea, Liwiti, Likawage na Mchakama vimeweza kuvuna magogo yenye mita za ujazo **458.2** na kuyachakata kwa Mashine ya kisasa inayohamishika na yenye ufanisi mkubwa iliyopatikana kuititia ufadhilli wa WWF na kuwezesha kupata Mapato ya Tshs **256,165,200/=** yaliyotokana na kuuza mbao. Kama Vijihi vingeza magogo pekee vingepata Tshs **120,303,800/=** tu. Hivyo kwa kuuza mbao vijiji vimeweza kupata maradufu ya faida ya ukilinganisha na uuzaaji wa magogo.
3. Shughuli za uchakati wa mbao katika maeneo ya vijiji yaliyofanya uchakati ilitoa ajira za muda mfupi kwa wanajamii takribani 105 katika kipindi cha uchakataji. Aidha wanajamii nane (8) kutoka kwenye vijiji vinne vya wilaya ya Kilwa wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya namna ya kutumia mashine hiyo.
4. Mpaka sasa vijiji 6 vimeweza kupanda jumla ya miti 1,696 ya Matunda (Mipapai, Michungwa na Miembe), 79,030 ya Biashara (Mkongo, Mpingo, Mnungunungu na Mkangazi).
5. Kijiji cha Nanjirinjiri A kimejenga Nyumba ya kulala wageni kama mradi wa maendeleo wa kijiji wenye thamani ya shilingi 107,000,000/= .

6. Vijiji vya Likawage, Nanjirinji A, Mchakama, Ngea, Kisangi, Liwiti na Nainokwe vimejenga Ofisi za vijiji pamoja na kununua samani zake
7. Vijiji vya liwiti, Mchakama, Ngea, Kisangi na Nanjirinji A vimeweza kujenga ofisiza Vijiji, nyumba za walimu, na wahudumu wa Afya, vyumba vya madarasa.
8. Vijiji vya Likawage, Ngea, Liwiti vimetengeneza madawati pamoja na kukarabati visima vya maji.
9. Ujenzi wa vyoo shule za msingi na sekondari kwa vijiji vya Liwiti, Likawage, Nanjirinji A, Ngea na Kikole.
10. Vijiji vya Likawage na Kisangi vimeweza kutoa msaada wa fedha kwa wahanga wa mafuriko katika vijiji vyao.
11. Kulipia Bima za Afya kwa kamati za maliasili na wazee wasiojiweza Nanjirinji A, Liwiti, Kisangi, Likawage, Kipindimbi na Kikole
12. Katika jitihada za kunusuru vifo vya wamama wajawazito na watoto/kabla/wakati na baada ya kujifungua vijiji vya Nanjirinji A na Liwiti vimekuwa vikichangia kiasi cha shilingi 50,000/- kwa jumla ya wamama wajawazito 470 (Nanjirinji A 400 na Liwiti 70).
13. Ununuzi wa sola kwa ajili ya zahanati ya Mchakama
14. Kuchangia sare kwa wanafunzi wa shule ya msingi na kiasi cha pesa cha sh.100,000/=kwa kila mwanafunzi anayefaulu kujeunga na sekondari kwa vijiji vya Nanjirinji A, liwiti na Likawage
15. Kusaidia wanafunzi wa shule za msingi kupata chakula. Mfano liwiti, Nainokwe na Ngea
16. Kulipa posho za walimu wa shule za awali kwa Nanjirinji A
17. Kuchimba visima vya maji Kikole, Kipindimbi
18. Vijiji kuweza kujigharamia katika shughuli za usimamizi wa misitu kama vile kufanya tathimini ya mazao ya Misitu, kufanya doria, kununua vyombo vya usafiri yaani pikipiki na kununua Sare za kamati ya Maliasili
19. Uelewa wa wanajamii juu ya usimamizi shirikishi wa misitu, utawala bora na matumizi ya fedha umeongezeka kutokana na elimu inayotolewa na Halmashauri ya Wilaya ikishirikiana na mashirika ya WWF, MJUMITA na MCDI na kupelekea kila mwanajamii kuwa mlinzi wa maliasili.

**C. CHANGAMOTO, JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA NA MAPENDEKEZO**

<b>S/N</b>	<b>CHANGAMOTO</b>	<b>JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA</b>	<b>MAPENDEKEZO</b>
1	Kukosa soko la uhakika la mazao ya misitu.	<ul style="list-style-type: none"> <li>Vijiji kuendelea kukaa na wafanya biashara katika kuelezea ubora na wingi wa rasilimali zao zilizopo katika misitu ya hifadhi ya vijiji.</li> <li>Kushirikisha wadau mbalimbali katika kutangaza soko la mazao ya misitu iliyopo katika misitu ya vijiji.</li> </ul>	Taasisi za serikali itoe kipaumbele kununua mazao ya misitu kutoka kwenye misitu ya hifadhi ya vijiji katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili kukuza soko la ndani la mazao ya Misitu.
2	Uhaba wa vitendea kazi wakati wa shughuli za usimamizi wa misitu kama vile pikipiki, sare, na sanduku la huduma ya kwanza hasa katika vijiji vya Nanjirinji B, Kipindimbi na Namatewa.	Katika mipango kazi ya mwaka bajeti ya ununuzi wa vitendea kazi hupangwa	Serikali na wadau mbalimbali wasaidie kutafuta wateja wa mazao ya misitu ili kupata fedha ya ununzi wa vitendea kazi.
3	Uvamizi wa Mifugo, wakulima na wavuanji haramu ndani ya misitu ya hifadhi ya vijiji.	Vijiji vimefanya doria mbalimbali kukabiliana na wafugaji, wakulima na wavunaji haramu ndani ya Misitu ya hifadhi ya vijiji.	Doria shirikishi zinazohusisha wananchi, watumishi wa sekta na taasisi mbalimbali zifanyike mara kwa mara.
4	Ukosefu wa mbinu mbadala na silaha za kujikinga na wanyama wakali kama vile tembo wakati wa shughuli mbalimbali za usimamizi wa misitu.	Vijiji vimekuwa vikitumia mgambo wa Kijijini amba ni wachache na wana majukumu mengine ya kijijini.	Wanakamati wapatiwe mafunzo ya mgambo hii itasaidia kijilinda na wanyama pamoja na majangili.

## **TAARIFA YAUSIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITUYA JAMII WILAYA YA LIWALE**

### **A. UTANGULIZI**

Mh. Mgeni rasmi

Ifuatayo ni taarifa fupi ya maendeleo ya vijiji vinavyotekeleza usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii katika Halmashauri ya wilaya ya Liwale, mkoa wa Lindi. Halmashauri ya wilaya kwa kushirikiana na shirika la kuhifadhi Mpingo na maendeleo (MCDI) kupitia ufadhlili wa mradi wa LIMAS na baadae programu ya kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu (FORVAC) iliwezesha utengaji wa misitu na uandaaji wa Mipango ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu 22 kati ya mwaka 2013 hadi 2020. Jumla ya hekta za misitu 211,451 zimehifadhiwa kisheria katika ardhi ya vijiji 22.

### **B. MAFANIKIO**

Mh. Mgeni rasmi, mafanikio yaliyotokana na usimamizi shirikishi wa misitu ni kama:

1. Kijiji cha Kibutuka kimechangia ujenzi wa Soko la Kijiji.
2. Vijiji vya mtawatawa, Mihumo, Barikiwa, Turuki, Mikuyu, Mikunya, Ngongowele, Nahoro, Mtungunyu, Likombora, Ngunja na Kitogoro vimenunua pipipiki na vitendea kazi vingine kama vile sare za kamati ya Maliasili na balskeli kwa kwaajili ya shughuli mbalimbali za usimamizi wa misitu.
3. Vijiji vya Nahoro, Mtungunyu, Kibutuka, Kitogoro na Mtawatawa vimechangia jumla ya takribani Tshs 11,500,000/= katika ujenzi wa kituo cha afya cha Kibutuka.
4. Vijiji vya Ngunja, Kitogoro, Kiangala, Mtawatawa, Litou, Ngongowele, Mikuyu, Nahoro, Mtungunyu, Nangano, Mihumo, Likombora, Turuki, Darajani, Mikunya na Legezamwendo vimechangia katika ujenzi wa vyumba vya madarasa ya shule za sekondari.
5. Kijiji cha Mtawatawa kinamlipa posho mwalimu wa kujitolea katika shule ya Msingi Mtawatawa.
6. Ujenzi wa vyumba vya madarasa ya shule za msingi (Ngongowele na Mikuyu 3, Kitogoro 1, Mtawatawa 1, Nahoro na Mtunguyu 3).
7. Vijiji vya Turuki na Mtawatawa vimechangia katika ujenzi wa zahanati za vijiji, na kijiji cha Nangano kimechangia ujenzi wa nyumba ya mganga.
8. Vijiji vya Mtungunyu, Nahoro, Mikuyu, Ngongowele, Ngunja, Mihumo na Mikunya vimejenga ofisi za Vijiji pamoja na ununuvi wa samani za ofisi.
9. Kijiji cha Nahoro kimeweka umeme wa nishati ya jua (sola) katika zahanati ya kijiji.

10. Kijiji cha Mtawatawa kimefanikiwa kununua trekta lenye thamani ya shilingi milioni 75 ambalo linarahisisha shughuli za kilimo na kuongeza pato la kijiji.
11. Vijiji vya Mtawatawa, Kitogoro na Mikunya vimeweza kugharamia zoezi la kufanya tathimini shirikishi ya rasilimali za misitu na kuandaa mpango wa usimamizi na uvunaji endelevu.
12. Vijiji vya Mtawatawa, Mikunya na Nangano, vimejenga Nyumba ya Mtendaji wa kijiji.
13. Kijiji cha Mtawatawa kimegharamia uchimbaji wa kisima cha maji na kijiji cha Kitogoro kimechangia ujezi tanki la kuhifadhia maji katika shule ya msingi Kitogoro.
14. Kijiji cha Barikiwa kimechangia ujenzi wa matundu manne (4) ya vyoo ya shule ya msingi Barikiwa na Vijiji vya Mtungunyu na Nahoro vimechangia katika ujenzi wa vyoo vya ofisi za vijiji.

## C. CHANGAMOTO

Mh. Mgeni rasmi, pamoja na mafanikio haya, vijiji hivi bado vinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

S/N	<b>CHANGAMOTO</b>	<b>JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA</b>	<b>MAPENDEKEZO</b>
1	Ukosefu wa masoko ya uhakika ya mazao ya misitu hasa kwa jamii ya miti isiyofahamika.	Vijiji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali vinaendelea kutafuta wateja ili waweze kununua mazao ya misitu.	Taasisi za serikali itoe kipaumbele kununua mazao ya misitu kutoka kwenye misitu ya hifadhi ya vijiji katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili kukuza soko la ndani la mazao ya Misitu.
2	Ongezeko la matukio ya uvamizi wa wanyamapor wakali na hatari kwa maisha ya binadamu wakati wa kufanya doria.	Baadhi ya vijiji vimeanza mchakato wa kurejeshewa silaha za moto (Bunduki) ambazo awali zilikuwepo ili zitumike katika kujikinga na wanyama wakali na hatari kwa maisha ya binadamu.	Kamati za Maliasili za vijiji zipatiwe mafunzo ya jeshi la akiba (mgambo) yatakayosaidia kuongeza mbinu za matumizi ya silaha na kuongeza ukakamavu ili kukalibiana na matukio ya uvamizi wa wanyama wakali na wavunaji haramu.
3	Uhaba wa vitendea kazi vya kuendeshea shughuli za usimamizi wa misitu hasa kwa vijiji ambavyo havijavuna mazao ya Misitu.	Katika mipango kazi ya mwaka bajeti ya ununuzi wa vitendea kazi imepangwa	Serikali na wadau mbalimbali wasaidie kutafuta wateja wa mazao ya misitu ili kupata fedha ya ununuzi wa vitendea kazi.
4	Uvamizi wa Mifugo, wakulima na wavuanji	Vijiji vimefanya doria za mara kwa	Doria shirikishi zinazohusisha

	haramu ndani ya misitu ya hifadhi ya vijiji.	mara ili kukabiliana na wafugaji, wakulima na wavunaji haramu ndani ya Misitu ya hifadhi ya vijiji.	wananchi, watumishi wa sekta na taasisi mbalimbali zifanyike mara kwa mara.
--	--	---	---

## **TAARIFA YA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU YA JAMII WILAYA YA RUANGWA.**

### **A. UTANGULIZI**

Mh Mgeni rasmi

Ifuatayo ni taarifa fupi ikiwa ni majumuisho ya taarifa zitokanazo na shughuli za uhifadhi kwenye vijiji 6 vya Wilaya ya Ruangwa Mkoa wa Lindi.

Wilaya ya Ruangwa ni mionganini mwa Wilaya sita zilizopo mkao wa Lindi. Halmashauri ya Wilaya, TFS kwa kushirikiana na mashirika ya Indufor na MCDI ilitekeleza mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii kuanzia mwaka 2004. Baadae mwaka 2019 Programu ya kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao ya misitu (FORVAC) iliendeleza shughuli za usimamizi shirikishi wa misitu. Jumla ya hekta za misitu **21,139** zimetengwa na kuhifadhiwa kisheria katika vijiji 6 (Ng'au hekta 4145, Nandenje hekta 5025, Nahanga 3076, Lichwachwa 2,447, Mmawa 446 na Mchichili 6,000).

### **B. MAFANIKIO**

Mh. Mgeni Rasmi;

Yafuatayo ni mafanikio yatokanayo na usimamizi shirikishi wa misitu;

1. Ununuzi wa trekta 5 za vijiji (Ng'au, Mchichili, Lichwachwa, Nahanga, na Nandenje)
2. Ujenzi wa ofisi za vijiji; Mchichili, Nahanga, Ng'au, Lichwachwa na Nandenje.
3. Ujenzi wa zahanati ya Kijiji cha Nandenje, Kujenga madarasa 2 Kijiji cha Mchichili, madarasa 3 kijiji cha Nahanga na madarasa 2 Kijiji cha Lichwachwa kuchangia ujenzi wa madarasa 2 Kijiji cha Ngau,
4. Kijiji cha Ng'au kimechangia ujenzi wa vyoo 2 vya shule ya msingi( Mnacho 1 na Mbungu 1).
5. Ujenzi wa choo cha zahanati Nandenje.
6. Kijiji cha Ngau kimetengeneza madawati 20 ya shule ya msingi Mbungu na kukarabati madawati 40 katika shule ya msingi Mnacho.
7. Ujenzi wa Nyumba 1 ya mganga kijiji cha Nandenje na Nyumba 2 za walimu Kijiji cha Lichwachwa na Ng'au.
8. Kijiji cha Ng'au kimechangia chakula cha wanafunzi 130 kwaajili ya kambi za masomo shule za msingi na sekondari.
9. Kuchangia ununuzi wa mashine ya kudurufu ( photocopy mashine) shule ya wasichana Lucas Maria Kijiji cha Ng'au,
10. Ununuzi wa betri moja ya sola kwa ajili ya wodi ya wazazi katika zahanati ya Mnacho katika kijiji cha Ng`au.
11. Ujenzi wa kizimba cha kuchomea takataka za zahanati katika Kijiji cha Nandenje
12. Ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao ya kijiji cha Nahanga

13. Ununuzi      wa      nyumba      ya      mganga      Kijiji      cha      Lichwachwa

## C. CHANGAMOTO, JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA NA MAPENDEKEZO

Mh Mgeni Rasmi:

Pamoja na mafanikio tajwa hapo juu vijiji hivi vimekuwa vikipitia changamoto zifuatazo katika usimamizi shirikishi wa misitu ya hifadhi ya vijiji;

	<b>CHANGAMOTO</b>	<b>JITIHADA ZILIZOCHUKULIWA</b>	<b>MAPENDEKEZO</b>
1	Upungufu wa vitendea kazi kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa misitu	Vijiji vimeandaa mpango na bajeti wa mwaka ulioorodhesha mahitaji yote yanayotumika katika usimamizi wa misitu.	Serikali na wadau mbalimbali wasaidie kutafuta wateja wa mazao ya misitu ili kupata fedha ya ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya usimamizi wa misitu.
2	Uchomaji holela wa misitu.	Doria za mara kwa mara na kutoa elimu ya moto kwa wanajamii.	Serikali na wadau mbalimbali wa uhifadhi kutoa mafunzo kwa kamati za maliasili za vijiji na wanajamii kuhusu ubabuaji ili kupunguza matukio ya moto kichaa kipindi cha kiangazi.
3	Uvamizi wa Mifugo, wakulima, wawindaji na wavunaji haramu ndani ya misitu ya hifadhi ya vijiji.	Vijiji vimefanya doria mbalimbali kukabiliana na wafugaji, wakulima, wawindaji na wavunaji haramu ndani ya Misitu ya hifadhi ya vijiji.	<ol style="list-style-type: none"> <li>Kamati za Maliasili zipatiwe mafunzo ya mgambo hii itasaidia kujilinda na uvamizi wa wafugaji, wakulima, wawindaji na wavunaji haramu ndani ya misitu ya hifadhi ya vijiji.</li> <li>Doria shirikishi zinazohusisha wananchi, watumishi wa sekta na taasisi mbalimbali zifanyike mara kwa mara.</li> </ol>
4	Upungufu wa wateja wa mazao ya misitu kwenye misitu ya vijiji.	Vijiji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali vinaendelea kutafuta wateja ili waweze kununua mazao ya misitu.	Taasisi za serikali zitoe kipaumbele kununua mazao ya misitu kutoka kwenye misitu ya hifadhi ya vijiji katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili kukuza soko la ndani la mazao ya misitu.

## **TAARIFA YA WANAJAMII KUTOKA MOROGORO, MVOMERO NA KILOSA WARSHA YA WADAU WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU**

### **DHIMA: MCHANGO WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU KATIKA KUTEKELEZA MIPANGO NA VIPAUMBELE VYA SERIKALI YA AWAMU YA TANO YA UCHUMI WA VIWANDA ILIYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA NALUNGOMBE, RUANGWA**

Ndugu Mgeni Rasmi

Ndugu wa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya

Ndugu washiriki wa Warsha

#### **1. UTANGULIZI- Upokeaji wa Mradi wa Uhifadhi wa Misitu ya Asili ya Vijiji**

Mradi wa Uhifadhi wa Misitu ya Asili katika Mkoa wa Morogoro ulianza tangu mwaka 2012 na umeshatekelezwa kwa awamu ya tatu. Awamu ya kwanza uliitwa Mradi wa Mkaa Endelevu (2012-2015), Awamu ya Pili Uliitwa Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania (2015-2019) na sasa Awamu ya Tatu ya mradi wa CoForEST (2019-2022) zote zikifadhiliwa na Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC). Utekelezaji umefanyika na Mashirika ya TFCG na MJUMITA kwa ushirikiano wa Karibu na wadau wa Wilaya za Kilosa, Morogoro, Mvomero (Mkoa wa Morogoro), Wilaya za Kilolo, Nachingwea, Liwale na Ruangwa. Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zake, OR-TAMISEMI, Halmashauri za vijiji.

#### **3. UTEKELEZAJI WA MRADI**

Tangu mwaka 2012, Mradi umetekelozwa katika vijiji 30 Mkoa wa Morogoro. Baada ya kufanya utambuzi na uhamasishaji. Vijiji vyote hivi vilianza na mchakato wa

- Kuandaa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ambapo tulitenga maeneo ya vijiji kwa matumizi mbalimbali vijijini ikiwa Pamoja na kutenga maeneo ya Hifadhi za Misitu ya vijiji. Vijiji vyote 30 vilipitia mchakato huu na kukamilisha katika ngazi za wilaya na sasa wanatekeleza.
- Kutenga Maeneo ya Misitu kwa ajili ya uvunaji- Maeneo ya misitu yaliyotengwa yamo na ya uvunaji endelevu wa mazao ya misitu hususan Mkaa na mbao. Asilimia 10 ya maeneo ya misitu yaliyotengwa ndo yanafanyiwa uvunaji endelevu wa mkaa na asilimia 90 iliyobaki inaendelea kuhifadhiwa kwa shughuli nyingine.

#### **4. MAFANIKIO YA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU**

Kwa utekelezaji wa mradi huu Mkoa wa Morogoro, jamii na Halmashauri zimenufaika kwa mambo mengi ikiwa ni pamoja na yafuatayo;

- i. Vijiji 30 kuwa na mipango ya Matumizi Bora y Ardhi ambayo inatekelezwa. Ikiwa na sheria ndogo za utekelezaji. Hii imechangia vijiji hivi kupata Masjala za Ardhi 30 (ambako ofisi za vijiji zimepatikana)
- ii.

- iii. Misitu 30 ya Wilaya ya Morogoro imefanikiwa kukamilisha mchakato wa Kutangaza misitu ya Hifadhi ya vijiji kupitia ushirikiano mkubwa na Idara ya Misitu na Nyuki kwa Tangazo na. (GN 688) ya mwaka 2020
- iv. Vijiji kuwa na mapato kifedha kupitia uvunaji endelevu wa mazao ya misitu hasas Mkaa na mbao kutoka katika Hifadhu za Misitu ya vijiji wanayoitunza.
- v. Vijiji vimetekeleza miradi ya vipaumbele katika maeneo yao kutokana na mapato ya uvunaji wa mazao ya misitu kwa njia endelevu. Hadi kufikia Novemba 2020 Jumla ya fedha za kitanzania 321,102,997 zimewekezwa kwenye miradi ya maendeleo ya jamii katika vijiji 30, miradi hii imemalizika na mingine inaendelea kutekelezwa katika Wilaya ya Morogoro, Mvomero na Kilosa. Baadhi ya miradi hii ni kama
  - Kuwalipia wananchi bima ya afya (CHF)
  - Ujenzi na ukarabati wa Zahanati za vijiji na nyumba za wagagnga Pamoja na vifaa vya hospitali
  - Miundo mbinu ya barabara kama kule Kijiji cha Ihombwe
  - Miundo mbinu ya maji safi na uchimbaji, usambazaji wa maji safi
  - Madarasa, ujenzi wa nyumba za waalimu na vyoo vya Watoto mashulen
  - Ulinzi wa misitu na shusghuli za uhifadhi na miradi mingine mingi
- i. Kuboresha utawala bora kwa kuwajengea uwezo wanajamii wakiwemo, wajumbe wa Halamashauri za vijiji, Kamati za Maliasili za vijiji, Kamati za Matumizi bora za ardhi kamati za doria.
- ii. Jamii hasa mtu mmoja moja wakiwemo wanawake kupata haki miliki za kimila katika kurasimisha ardhi.

### **Fursa Zilizopo**

1. Kuna fursa ya wazalishaji wa mkaa kwa njia endelevu kupata mafunzo na utaalamu wa namna bora ya uzalishaji wa mkaa kwa njia endelevu
2. Kwa kutofanya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii katika vijiji, Hal mashauri na wananchi wasingegundua faida na manufaa ya misitu hiyo. Mchango wa USM umeonekana Dhahiri kwenye sekta mbalimbali vijijini mfaano Afya, Elimu, ujenzi na maendeleo ya wananchi.
3. Kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa kumeongeza sana ushiriki wananchi katika shughuli mbalimbali na hawaangalii sana misitu kuwa chanzo kikuu cha mapato. Hii ni Pamoja na vikundi vya ufugaji wa nyuki.
4. Kuna misitu mingi sana bado ambayo hajahifadhiwa, hii ni fursa kwa vijiji na Wilaya kuungeza wigo na kutengeneza fursa za mapato katika Wilaya na vijiji.

### **CHANGAMOTO ZA USM**

1. **Utawala bora katika vijiji-** vijiji ambavyo viko kwenye USM na mradi vimepata fursa ya kuwezesha na kupata elimu ya masuala mbalimbali ya usimamizi shirikishi wa Misitu. Hata hivyo, kamati nyingi zimebadilishwa na wajumbe sasa ni wapya. Hawana

mafunzo na wanapelekea kutosimamia na kufuata taratibu. Mwanya wa udhaifu wa usimamizi unaendelea hap ana kuchangia usimamizi hafifu.

2. **Wingi wa Mifugo**- katika maeneo ya Morogoro, wafugaji wamekuwa wakihamahama na kuchangia misitu mingi kuvamiwa na kuongeza migogoro na wakulima karibu na maeneo hayo. Uelimishaji ukiendelea na usimamizi wa sheria za matumizi bora ya ardhi kunaweza kusaidia kupunguza changamaoto hii. Hata hivyo, katika maeneo yaliyovunywa , machipukizi yanatishiwa kukua kutokana na kuharibiwa na mifugo.
3. **Utekelezaji wa Tangazo la Serikali (GN 417)**. Katika maeneo mengi kulikuwa na katazo la kufanya biashara endelevu ya mkaa na mbao. Hii ilipelekea maoato mengi katika vijiji hivi kushuka sana. Hii inapelekea uharibifu kuendelea katika maeneo mengine hasa yale ambayo hayana usimamizi na hivyo kuendelea kutishia uwepo wa misitu hii.

### **MAOMBI**

1. Tunaomba vijiji ambavyo vimeshaingia kwenye utaratibu wa USM na kutekeleza visihuishwe kwenye GN 417.
2. Halmashauri za Wilaya na vijiji vitambue na kuanisha maeneo yote ambayo yana misitu ambayo hajasimamiwa na kuifanya utaratibu wa kusimamiwa (Mipango ya usimamizi na mipango ya uvunaji) kwa ajili ya kueneza dhana ya USM katika maeneo mengi Zaidi.

FCG •